# JINSI YA KUTUMIA STRATEGIC IMPACT UINJILISTI ZANA







1. Kushiriki ushuhuda wako wa:
   - Toa ushuhuda wa maisha yako yalivyo kuwa KABLA ya kumwamini kristo Yesu,
   - Jinsi ulivyofikia hatua ya kumwamini mwokozi.
   - Jinsi maisha yako yalivyobadilika baada ya kumwamini Yesu kwa ajili ya wokovu.

<u>**Waonyeshe sehemu ya mbele ya zana.**</u>

**Sema:** *"Naomba niwaulize maswali machache kuhusu mulivyoamini na kuwaonyesha kwenye Biblia jinsi ya kuwa na uhakika wa kuwa na uzima wa milele?"*

2. Waonyeshe pembe tatu na waambie kwamba umbo hili linawakilisha Mungu. Uliza, *"Je unamwamini Mungu? Je unaamini kwamba anakupenda wewe?"* Subiri mtu ajibu maswali haya yatakuwezesha wewe ***kufanya mazungumzo*** na mtu badala ya wewe tu kuongea kwao.

3. Ni **muhimu kusoma andiko kwenye Biblia** sambamba na kila umbo. Anza na ***Yohana 3:16*** **(1)**
   - Uliza kama mtu anabiblia, kama anayo msaidie kumwonyesha mahali ambapo hili andiko lipo kwenye Biblia.
   - Itakuwa vizuri kama huyo mtu atasoma mwenyewe hilo andiko. Hata hivyo uwe makini kama hawawezi kusoma. Kama watasita na kusema kwamba, sina miwani ya kusomea soma wewe kwa niaba yao.

4. Waonyeshe umbo la mtu hapo chini katika jedwali la kwanza. Uliza, **"Unadhani huyu mtu anawakilisha nani?"** Wanaweza kusema anawakilisha "watu" au " Ibilisi" au watu wengine. Waambie kwamba hili umbo linawakilisha kila mtu duniani wewe mimi na kila mtu. Onyesha hiyo sehemu nyeusi ambayo inaonyesha kwamba watu wametengwa na Mungu. Soma *Warumi 3:23* **(2)** and ask, **"*Biblia inasema kwamba tumetengwa na Mungu sababu kila mmoja wetu ametenda dhambi je unaamini kwamba umemtenda Mungu dhambi?*"**

5. Soma *Warumi 6:23* **(3)** katika ile sehemu inayoonyesha watu walivyotengwa na Mungu. Kisha uliza, **"Je unaamini kwamba dhambi zako zimesababisha mauti – kutengwa na Mungu milele?"**




6. Geuza upande mwingine unaoonyesha msalaba. Soma *Warumi 5:8* **(4)** kisha sema, “**Mungu anatupenda na amefanya njia kwa ajili yetu kumjua yeye kwa kumtuma mwanae, Yesu kristo, kufa msalabani ili kulipa deni la dhambi zetu. Je unaamini kwamba Yesu alikufa kwa ajili yako?**”

7. Soma *Yohana 14:6* **(5)** na uliza, “**Je unaamini kwamba Yesu kristo ni njia pekee ya kupata uzima wa milele kwa Mungu?**”

8. Soma *1 Wakoritho 15:3-8* **(6)** kisha uliza, “**Je unaamini kwamba Mungu alimfufua Yesu kutoka wafu?**”

9. Geuza sehemu ya tatu na uwaonyeshe picha ya zawadi kisha sema, “**Mungu anataka upate uzima wa milele na ndiyo maana anakupa zawadi hii bure.**” Kisha soma *Waefeso 2:8-9* **(7)** kisha sema, “**Kama unaamini jina la Yesu, Mungu anakupa fulsa ya kuwa mtoto wa Mungu.**” Kisha soma *Yohana 1:12* **(8).**




10. “**Mungu anasema hivi kwa wale wanaokataa zawadi yake:**” soma *(2 Wathesalonike 1:8-10)* **(9). Lakini, “kama utaikubali hii zawadi kwa Imani Mungu ameahidi utapata uzima wa milele.”** *(1 Yohana 5:11-12)* **(10).**

11. **ULIZA: “Je utapenda kuipokea hii zawadi ya uzima wa milele kwa kumwamini Yesu kristo leo?”**

12. Kama jibu ni “**Ndiyo**,” soma *Warumi 10:9-10* **(11)**. unaweza kumpokea kristo kwa Imani leo kwa **kumwamini** moyoni mwako na **kumkiri** kwa kinywa chako. Maombi hayakuokoi wewe. Isipokuwa ni ***Imani yako kwa kristo*** ndiyo itakayokuokoa. Maneno ya maombi yanaweza kukusaidia kuonyesha Imani yako hapa kwa mfano wake: *“Bwana Yesu, nakuhitaji nakiri kwamba nimekutenda dhambi. Tafadhari nisamehe dhambi zangu Napokea zawadi yako ya kusamehewa dhambi na kupokea uzima wa milele leo kwa. Imani Ameni.”*

Jina ________________________

Anwani ______________________

_______________________________

_______________________________

Simu ________________________

Tarehe _____________ Umri _____

☐ Leo nampokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi

☐ Nataka kujua jinsi ninavyoweza kukua kiroho Katika imani ndani ya Kristo.

Siku __________ Muda __________

☐ Ninapenda kujifunza Biblia na watu Wengine/majirani.

Mwinjilisti/Mshuhudiaji:

__________________________________

__________________________________

13. Baada ya mtu kupokea zawadi ya Mungu ya uzima wa milele, uliza, **"Je umemwamini kristo kukusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele?"** Watie moyo katika Imani yao mpya kisha waombee.

14. Chana sehemu ya mwisho ya zana ya uinjilisti ya SI kusanya taarifa zao na tiki sehemu husika katika visanduku.

15. Kama inawezekana panga muda wa kuonana nao kesho ili kuanza kuwafundisha waamini wapya kwa kutumia zana ya uinjilisti ya SI kwa kugeuza nyuma kipeperusha.

16. Taarifa za mawasiliano na anwani za waamini wapya mpatie kiongozi mpya wa seli ambayo imeanzishwa.